**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA

**Juni, 2026**

**RUKWA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2026**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0755 279 058**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0758508982**

**Patron: 0755747429**

**Shule ya Sekondari sumbawanga**

**S.L.P. 737**

**Tarehe 10/05/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2026/2027**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2026/2027** na atasoma tahasusi ya **HGK/HKL**

Shule ya Sekondari Sumbawanga ni **Bweni** na ipo umbali wa km 1 Magharibi mwa mji wa Sumbawanga. Usafiri wa Bajaji ni Tsh 2,000/= toka stendi kuu na Bodaboda ni Tsh 5,000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ..................., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………… **.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule ni Shati mikono mirefu nyeupe mbili (2).
ii. Suruali mbili (2) moja Kijani nyeusi na Blue bahari.
iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
iv. Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
v. Tisheti (2) mbili (Zinapatikana shuleni kwa Tsh 15,000 kila moja)
vi. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
vii. Sweta rangi dark blue (blue nyeusi)
viii. Sare ya michezo ni tracksuit rangi ya blue nyeusi (dark blue) pamoja na jezi ya rangi ya blue.
ix. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

**2.1.1 sare za kazi (Shamba Dress)**

i) Suruali nyeusi moja
ii) Suruali ya khaki moja

**ANGALIZO: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari saba (07) (counter books) ziwe kwaya 3 na zaidi;
ii. **Ream 2 (A4)** kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.( Imeambatanishwa)
iv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko (kila mwanafunzi).
v. Mifagio 2 Wa ndani na wa nje (kila mwanafunzi)
vi. Moper, dryer na squeezer (kila mwanafunzi).
vii. Fyekeo 1, jembe 1 (wanafunzi wa HGK)
viii. Reki 1, panga 1 (wanafunzi wa HKL)
ix. Vyombo vya chakula sahani, bakuli kijiko na kikombe.
x. Mashuka mawili ya blue, branketi moja zito, foronya moja godoro (2 ½ x 6) na chandarua.

**Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ilipwe kupitia account ya shule ambayo ni (Elimu ya kujitegemea Sumbawanga Sekondari 62102501688 NMB) isipokuwa mchango wa nembo na kitambulisho.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote

inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

  **Mwanafunzi ambaye hana kadi ya BIMA YA AFYA anapaswa aje ni sh,50,400/=kwaajili ya ukataji wa BIMA YA AFYA pindi anaporipoti shule**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi na mzazi.
iii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SUMBAWANGA SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule KEVAS MASAWE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………….**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755 279 058**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0758508982**
- **Mwandamizi Taaluma 0755880778**
- **Mwandamizi Malezi 0756 632 327**

KIAMBATA ‘A’

SUMBAWANGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 737,
SUMBAWANGA.

FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical officer in respect to all of entrants

Student’s full name………………………………………………..

Age……………………..Sex…………………

Blood count ( red and whites)……………………………

Stool examination………………………………..

Urine analysis………………………….

Syphilis and other venereal diseases test……………………………………………
……………………………………………………………………..

TB test……………………………………………

Eye test………………………………………………………………………..

Ears……………………………………………………………………………..
………………………………..

Abdomen……………………………………………………………………..

Urine for plant test…………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

Defects,impotents (e.g.arms,legs etc) infections,chronic or family diseases etc.
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………………………………………….

I certify that the named above is fit to pursue further studies .

Station………………………………………………Signature……………………………..

Date…………………………………………Designation………………………………….

KIAMBATA ‘B’

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA SUMBAWANGA
SHULE YA SEKONDARI SUMBAWANGA

FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI

A.TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1.Jina la mwanafunzi …………………………………………
2.Tarehe ya kuzaliwa………………………………………….
3.Dini……………………………………………………….
4.Uraia…………………………………………………..
5.Mahali alipozaliwa…………………………………………….
6.Wazazi wote wapo hai?........................Kama ni hapana taja mzazi ambaye hayupo hai…………………..

B.TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1.Jina kamili…………………………………………
2.Kazi/Shughuli………………………………………
3.Uraia………………………………………………
4.Wilaya ya nyumbani………………………………
6.Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwanafunzi…………………………………………
……………………………………………………………………………………………
…………………………………………………….
7.Anwani ya nyumbani………………………………………………………..
8.Namba ya simu……………………………………………….
9.Ahadi ya mzazi/mlezi………………………………………………..
Mimi……………………………………………..naahidi kumtimizia mwanafunzi mahitaji yake yote ya shule kama yalivyoagizwa na shule pia naahidi kufuatilia maendeleo yak ya kitaaluma kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni.

Sahihi ya mzazi……………………………………….
Tarehe……………………………………
Jina la mzazi……………………………………….